

Taarifa kwa Umma

Imezuiwa hadi saa 5 asubuhi, 26 Juni 2013

## Wabunge wa vyama vidogo wanashiriki zaidi Bungeni

**26 Juni 2013, Dar es Salaam:** Uchambuzi wa utendaji wa Wabunge umeonyesha kwamba Wabunge wanaotoka katika vyama vidogovidogo na vyenye viti vichache huwa na wastani wa juu zaidi wa ushiriki. Tathmini hii inazingatia ushiriki uliofanywa na Wabunge katika miaka miwili ya kipindi cha ubunge cha 2010 – 2015. Wabunge wanaweza kushiriki kwa namna tatu: kwa kuuliza maswali ya msingi, maswali ya nyongeza na kutoa michango. Katika namna zote hizi, TLP ambacho kina mbunge mmoja na NCCR-MAGEUZI watano, vilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ushiriki kwa Mbunge. Hata hivyo, ukiondoa vyama vidogovidogo vyenye chini ya asilimia tano ya uwakilishi Bungeni, Chadema kinafanya vema zaidi, kikifuatiwa na CUF na CCM.

Matokeo haya yanatolewa katika muhtasari unaoitwa *Je, waliwajibika? Tathmini ya miaka miwili ya Bunge 2010-2012* uliyoandaliwa na Twaweza kwa kushirikiana na Centre for Economic Prosperity (CEP). Muhtasari unachambua data zinazopatikana kwenye tovuti ya Bunge, kuhusu ushiriki wa kila Mbunge wakati wa vikao vya Bunge. Bunge ndio mhimili wa demokrasia, likiwakilisha wapiga kura katika namna wanavyohusiana na dola. Twaweza na CEP zinatoa tathmini ya utendaji wa Wabunge kwa ujumla, kwa kila chama, kwa kila Mbunge na kwa aina ya ushiriki.

Tathmini inaonyesha kwamba Wabunge wa CCM walikuwa na ushiriki zaidi kwa ujumla, ingawa hili husababishwa na idadi kubwa ya viti vinavyoshikiliwa na CCM Bungeni. Hata hivyo, Wabunge wa CCM walikuwa idadi ndogo zaidi ya ushiriki kwa kila Mbunge mmojammoja. Jambo hili ni la kutarajiwa kwa Wabunge wa kutoka chama tawala, karibu wote wanaelekea kuwasilisha maslahi yanayofanana ya kitaifa. Hata hivyo, kwa maswali ya kisera katika ngazi ya jimbo, viwango vya shughuli zinatarajiwa kuwa sawa zaidi kwa kuwa kila Mbunge anawasilisha jimbo lake na maslahi ya jimbo hilo.

Jedwali hilo linaonyesha wastani wa michango kwa kila Mbunge kutoka katika vyama vyao husika.

	<b>Idadi ya Wabunge</b>	<b>Michango kwa kila Mbunge (jumla)</b>	<b>Maswali ya Msingi (kwa kila Mbunge)</b>	<b>Maswali ya Nyongeza (kwa kila Mbunge)</b>	<b>Michango (kila Mbunge)</b>
<b>Vyama Vikubwa</b>					
<b>Chadema</b>	48	57	6	11	40
<b>CUF</b>	35	41	5	8	28
<b>CCM</b>	254	39	3	6	30
<b>Vyama Vidogo</b>					
<b>TLP</b>	1	87	1	14	60
<b>NCCR-MAGEUZI</b>	5	74	7	17	50
<b>UDP</b>	1	37	0	9	28



Utendaji wa Wabunge pia ulitofautiana kulingana na kama walikuwa ni wa kuchaguliwa au wa kuteuliwa. Wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi na wale walioteuliwa na Rais walikuwa na ushiriki hafifu wakati wa vikao vya Bunge.

*"Wabunge wanachaguliwa ili watutumikie", alisema Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, "data hizi zinatupa zana muhimu ya kujua ni kwa kiasi gani wanatutumikia."*

*"Vikao vya Bunge vilivyopita vilirushwa moja kwa moja kupitia televisheni na wananchi walipata fursa ya kufuatilia majadiliano na kuona jinsi walivyokuwa wakiwakilishwa katika Bunge," alisema Thomas Maqway, Mkurugenzi Mtendaji, Centre for Economic Prosperity, "uwazi huu unalinda uadilifu na kuaminika kwa Bunge".*

Muhtasari unaendeleza dhima iliyochapishwa kwenye muhtasari mwingine wa Twaweza unaoitwa 'Je, waliwajibika?' uliotolewa mwaka 2010 na unaotoa uchambuzi linganifu wa ushiriki wa Wabunge Bungeni.

---Mwisho---

**Kwa taarifa zaidi:**

Risha Chande

Meneja wa Mawasiliano, Twaweza

**Barua pepe:** rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 665 7559

**Matini kwa Wahariri**

1. Data kamili zilizotumika kuandaa muhtasari huu zinapatikana kwenye tovuti ya Twaweza [www.twaweza.org/go/bunge2010-2012-swa](http://www.twaweza.org/go/bunge2010-2012-swa)
2. Muhtasari wa 2010 unapatikana kupitia [www.twaweza.org/uploads/files/Bunge%20session%2019-final-published.pdf](http://www.twaweza.org/uploads/files/Bunge%20session%2019-final-published.pdf)
3. Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayoamsha msukumo wa kiraia na ambayo inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika ya Mashariki. Twaweza inaamini kwamba mabadiliko ya kudumu huhitaji msukumo unaoanzia chini, na inatafuta kukuza hali na kupanua fursa ambazo kwazo mamilioni ya watu wanaweza kupata taarifa na kufanya mabadiliko hayo yatokee katika jamii zao na hasa kwa kuziwajibisha serikali moja kwa moja.
4. Centre for Economic Prosperity (CEP) ni taasisi ya utafiti yakinifu inayopanua uwezo wa kufikiri na mawazo kuhusu michakato ya kiuchumi inavyofanya kazi nchini Tanzania.
5. Unaweza kufuatilia kazi zaidi za Twaweza kupitia:

**Tovuti:** [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org) **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza\_NiSisi